KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 13, Issue 3

19th Ramadhân 1432

19th Aug, 2011

YALIYOMO

HADEETH DHA'EEF 1 - 3

NUKTA MUHIMU 3 - 4

Baadhi Ya Ahaadeeth Dhaifu Zinazonukuliwa Sana (Katika Mwezi Wa Ramadhân) Na: Sheikh al-Albâni (رحمه الله)

Kwa hakika Allâh (سبحانه وتعالى) ameiteulia Sunnah ya Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) wajumbe waadilifu wenye kuiondolea mageuzi ya watu wapotofu, na kuiondolea tafsiri za wenye kuvuka mipaka, na kuyafichua mambo ya batili yaliyolimbikizwa na waghushi (wenye kuichanganya haki na mambo duni).

Kwa miaka mingi uongezekaji mwingi umechanganywa nayo (sunnah), emma ahaadeeth zilizo dhaifu, za urongo au za kuzua na mfano wake na hayo yamefafanuliwa na kubainishwa kikamilifu na Wanavyuoni kwa miaka yote. Leo, mwenye kuangalia katika vitabu vya waandishi na maneno ya wahubiri ataona yakwamba hawajali hata chembe kuhusiana na suala hili isipokuwa wale waliorehemewa na Allâh, hata kama kunapatikana vitabu vya wanavyuoni vya marejeo, vyenye kuchambua ni zipi ahaadeeth zilizo swaheeh na kuzibainisha riwaya zilizo dhaifu.

Katika ufafanuzi wa mas'ala haya na athari zake mbovu juu ya 'ilmu na kwa watu, sisi hatukusudii kumshutumu au kumlaumu mtu yoyote. Sisi tutanukuu tu baadhi ya mifano ya riwaya zilizozuliwa mpaka zikawa ni zenye kujulikana au zikawa na umashuhuri miongoni mwa watu, kiasi cha kwamba hutokuwa ni mwenye kusoma makala au kusikiza mawaidha isipokuwa utasikiya ahaadeeth hizo dhaifu zikiwa na umashuhuri mkubwa ndani yake. Kwahiyo, kwa kuyafanya kazi maneno yake (صلى الله عليه وسلم): *"Fikilizeni kutoka kwangu hata kama ni aya moja tu ..."* [Imepokewa na Imâm al-Bukhâri (6/361).]

Na maneno yake (صلى الله عليه وسلم): *"Dini ni kunasihiyana ..."* [Imepokewa na Imâm Muslim (No. 55)]

Sisi twasema: Ahaadeeth zilizo dhaifu ambazo ni mashuhuri miongoni mwa watu, wa kila tabaka, ni nyingi sana, kiasi cha kwamba ni wachache wawezao kutaja chochote kilicho swaheeh – licha ya kuenea kwake pia. Rehma za Allâh (سبحانه وتعالى) zimshukie Imâm 'Abdullaah Ibn al-Mubaarak aliyesema: "Katika hadeeth iliyo swaheeh kuna utoshelevu kwahivyo hakuna haja ya kilicho dhaifu."

TANGAZO LA SWALA YA 'EID

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA

TUNAFURAHA KUWATANGAZIA SWALAATUL 'EID ITAKAYOSWALIWA KATIKA UWANJA WA CONGO BOYS [MBARAKI POLICE] MWEZI UTAKAPO-ONEKANWA KATIKA ULIMWENGU WA KI-ISLAMU. SWALA ITASWALIWA SAA MOJA NA NUSU 7:30 AM ASUBUHI. TWAWAOMBA MUJE NA MISWALA YENU NA WUDHU WENU IN-GAWA MAJI NA MIKEKA ITAKU-WEPO . NAFASI ZA WANAWAKE PIA ZITAKUWEPO, NAO WAJITOKEZE KWA WINGI KAMA ILIVYO SUNNAH YA BWANA MTUME MUHAMMAD (صلى الله عليه وسلم)

Kwahiyo, na awe Imâm huyu ni kielelezo kwetu, na tushikamane na 'ilmu iliyosafika na swaheeh.

Na katika hadeeth zilizo dhaifu ambazo ni kawaida ya watu kuzinukuu kuhusiana na Ramadhân ni:

1. *"***Lau kama waja wangeliujua Utukufu wa Ramadhân, basi Ummah wangu wangeliutamani mwezi wa Ramadhân kuwa ni mwaka mzima. Kwa hakika, Pepo imeandaliwa kwa ajili ya Ramadhân kuanzia mwanzoni mwa mwaka mpaka mwaka ufuatao..."** *Nayo ni hadeeth ndefu.*

Hadeeth hii imepokewa na Ibn Khuzaymah (No. 1886); Ibn al-Jawzee katika *Kitaab al-Mawdhoo'aat* (2/ 188-189); na Abu Ya'laa katika *Musnad* yake kama ilivyo katika *Al-Matwaalibul 'AAliyah* (46/a-b kwenye karatasi zenye khati zake) kwa njia ya Jareer Ibn Ayyub al-Bajalee: kutoka kwa ash-Sha'bee: kutoka kwa Naafi' Ibn Burdah: kutoka kwa Abu Mas'ood al-Ghifaaree.

Hadeeth hii imezuliwa (mawdhoo'), na sababu ni huyu Jareer Ibn Ayyub. Ibn Hajr amenukuu wasifu wake katika Lisaanul-Meezaan (2/101) na akasema: "Ni mashuhuri kwa udhaifu wake." Kisha akayanukuu maneno ya Abee Nu'aim kumuhusu yeye: "Alikuwa akizua ahaadeeth," kutoka kwa Al-Bukhâri: "Munkar katika kusimulia hadeeth," na kutoka kwa an-Nasaa'ee: "Aliyetupwa."!!

Ibn al-Jawzee akaihukumu kuwa ni ya kuzuliwa, na akasema Ibn Khuzaymah baada ya kuipokea: "Iwapo riwaya hii ni swaheeh, kwani kuna shaka ndani ya moyo kumuhusu Jareer Ibn Ayyub al-Bajalee."

2. **"Enyi watu, kwa hakika umewajilia nyinyi mwezi Mtukufu, mwezi ambao ndani yake muna**

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

usiku ulio bora kuliko miezi elfu moja. Allâh amefaradhisha kufunga ndani yake, na kusimama kwa swala katika usiku wake kuwa ni kitendo cha kukokotezwa. Yoyote mwenye kutaka kujikurubisha na Yeye kwa vitendo vyema ndani yake atakuwa ni kama mwenye kutekeleza kitendo cha wajibu katika miezi mengine… Ni mwezi ambao mwanzoni mwake Ni Rehma, Na katikati mwake Ni Msamaha, na mwishoni mwake ni kuwachwa huru na moto…"

Vilevile, hii ni hadeeth iliyo ndefu na sisi tumezinukuu sehemu zake zilizo maarufu sana.

Hadeeth hii vilevile imepokewa na Ibn Khuzaymah (No. 1887), al-Mahaamulee katika kitabu chake *Amaalee* (No. 293), na al-Asbahaanee katika *Targheeb* (Q/178, B- kwenye karatasi zenye khati zake) kwa njia ya 'Alee Ibn Zayd Ibn Jud'aan: kutoka kwa Sa'eed Ibn al-Musayyib: kutoka kwa Salmaan.

Isnaad hii ni dha'eef kutokana na udhaifu wa 'Alee Ibn Zayd. Ibn Sa'd amesema kumuhusu yeye, "Ana udhaifu ndani yake, hatumiwi kama ni dalili." Amesema Ahmad Ibn Hanbal: "hana nguvu." Ibn Ma'een akasema, "ni dhaifu." Akasema Ibn Abee Khaithumah: "ni dhaifu katika kila kitu." Ibn Khuzaymah akasema: "Mimi simkubali yeye kama dalili kutokana na fahamu zake zilizo dhaifu." – kama ilivyo katika *at-Tahdheeb* (7/322-323).

Ibn Khuzaymah amesema baada ya kunukuu riwaya yake: "Iwapo riwaya itakuwa ni swaheeh." Ibn Hajr akasema katika *al-Atraaf*: "Imesimuliwa na 'Alee Ibn Zayd al-Jud'aan peke yake na yeye alikuwa ni mtu dhaifu. Na kama alivyonukuu kutoka kwake as-Suyootee katika *Jam'ul-Jawaami'* (No. 23, 714). Ibn Abee Haatim amepokea kutoka kwa babake katika '*Ilalul-Hadeeth* (1/249) yakwamba amesema: "hadeeth hiyo ni munkar."

3. "Fungeni mutapata swiha njema."

Ni sehemu ya hadeeth iliyopokewa na Ibn 'Adiyy katika *al-Kaamil* (7/2521) kwa njia ya Nahshal Ibn Sa'eed: kutoka kwa adh-Dhahhak: kutoka kwa Ibn 'Abbaas.

Na Nahshal ametupiliwa mbali (*matrook*) kwa sababu alikuwa akisema urongo, na adh-Dhahhaak hakuwahi kupokea kutoka kwa Ibn 'Abbaas.

Na akapokea at-Twabaraani katika 'Al-Awswat' (1/Q, 69/ أ– *Majma' ul-Bahrain*), na Abu Nu'aim katika *'at-Twibb an-Nabawee'* kama ilivyo kwenye *'Takhreejul-Ihyaa'* (3/87), na Ibn Bukheyt katika *'Juz'ihi* – kama ilivyo kwenye *'Sherh al-Ihyaa'* (7/401) – kwa njia ya Muhammad Ibn Sulaymaan Ibn Abee Daawud, kutoka kwa Zuhayr Ibn Muhammad, kutoka kwa Suhayl Ibn Abee Swaalih, kutoka kwa Abee Hurairah.

Na sanad yake ni dha'eef, amesema Abu Bakr al-Athrum: "Nimemsikiya Ahmad akisema – nae akataja riwaya ya watu wa Shaam kutoka kwa Zuhayr Ibn Muhammad, akasema: 'Wamepokea ahaadeeth ambazo ni munkar kutoka kwake.'"

Akasema Abu Haatim: "Ana udhaifu Kwenye fahamu zake, ahaadeeth zake zilizopokewa akiwa Iraaq ni bora kuliko hadeeth zilizopokewa akiwa Shaam kutokana na udhaifu wa fahamu zake." Amesema al-'Ijlee: "Ahaadeeth hizi zilizopokewa na watu wa Shaam kutoka kwake si za kuniridhisha mimi," kama ilivyokuja kwenye *Tahdheebul-Kamaal* (9/417).

Nikasema: "Muhammad Ibn Sulaymaan ni mtu wa Shaam na unapatikana wasifu wake katika *Taareekh Dimishq* (15 Q, 386) – kwahiyo riwaya zake kutoka kwa Zuhayr, kama walivyoeleza wanavyuoni, ni munkar ambapo hadeeth hii ni mojawapo!!

3. "Mwenye kuacha kufunga siku moja katika mwezi wa Ramadhân pasi na udhuru unaostahiki, wala maradhi – basi hata Kama angelifunga milele, haitoweza kuilipa siku hiyo."

Hadeeth hii imenukuliwa kwa njia iliyokatika na al-Bukhâri katika swaheeh yake (Fat-hul-Baaree, 4/160) bila ya isnaad yoyote. Imeunganishwa na Ibn Khuzaymah katika swaheeh yake (No. 1987), at-Tirmidhee (No. 723), Abu Daawud (No. 2397), Ibn Maajah (No. 1672), an-Nasaa'ee katika *al-Kubraa* kama ilivyo kwenye *Tuhfatul-Ashraaf* (10/373), al-Baihaqee (4/228) na Ibn Hajar katika *'Taghleequt-Ta'leeq* (3/170) kwa njia ya Abul-Mutawwas: kutoka kwa babake: kutoka kwa Abu Hurairah.

Amesema Ibn Hajar katika Fat-Hul Baaree (4/161): "Wamekhalifiyana kiyasi kikubwa kwenye riwaya yao kutoka kwa Habeeb Ibn Abee Thaabit, nayo ina njia tatu za udhaifu:

Utata kwenye wapokezi wake.

Hali ya Abul-Mutawwas haijulikani.

Shaka iwapo babake alikutana na Abu Hurairah au laa."

Amesema Ibn Khuzaymah baada ya kuisimulia: "Ikiwa riwaya hii ni swaheeh, kwani mimi sina nijualo kumuhusu huyu Abul-Mutawwas wala babake." Kwahivyo hadeeth hii pia ni dha'eef.

Hizi ni ahaadeeth nne zilizothubutu kuwa ni dha'eef na zisizotegemewa na wanavyuoni, lakini bado twazisikiya na kuziona kila siku katika mwezi Mtukufu wa Ramadhân hususan, na pia kwenye nyakati nyengine. Ni dhahiri yakwamba baadhi ya ahaadeeth hizi zina sehemu zenye maana ya sawa na tena zikathibitishwa kwenye Sharee'ah, kwenye Kitaab na Sunnah. Hatahivyo, jambo hili kivyake halituruhusu sisi kunasibisha chochote na Mtume (صلى الله عليه وسلم) jambo ambalo halikuthubutu na kuswihi kutoka kwake, hususan, na kila aina ya Shukrani ni za Allâh, yakwamba hakika Ummah huu miongoni mwa Ummah zote zilizotangulia, ameuhusisha Allâh (سبحانه وتعالى) na isnaad. Na kwa isnaad hizo hujulikana anaekubalika kutokamana na aliyeingizwa, na swaheeh kutokamana na yaliyozuliwa. Ni mfumo wa tawi lililo madhubuti sana la 'ilmu iliyo swaheeh, na chembelecho aliyesema katika kulisifu tawi hilo: "'Ilmu ya yaliyopokewa na mizani ya kuswihi habari zake."

NUKTA MUHIMU ZINAZOHUSIANA NA 'IBAADA ZA MWEZI WA RAMADHAAN

Na: Sheikh al-Albaani

Ingawaje, majadiliano yetu yametupelekea kupita kiwango tulichokitarajia. Hili ni jambo lisiloweza kuepukika, kwa sababu limehitajika na Nyanja zote za utafiti wa ki-Uwanachuoni. Kwa ajili hii tumeamua kuwaletea wasomaji wetu waheshimiwa mukhtasari wa mas'ala yanayohusiana na 'Ibaada za Mwezi wa Ramadhaan, jambo ambalo litakalorahisisha ukaguzi wa haraka na utekelezaji wake—Insha-Allâh .

NUKTA MUHIMU

1. **KUSWALI TARAWEEH KWA JAMAA'AH NI SUNNAH:** Kuswali

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Taraweeh kwa Jamaa'ah ni sunnah na wala si Bid'ah. Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliiswali kwa Jamaa'ah kwa siku nyingi, na sababu ya kuwacha ilikuwa ni kuchelea tu kwa baadhi ya watu wake miongoni mwa Ummah wake huwenda wakadhania yakwamba hii ni swala ya waajib iwapo yeye angeliiendeleza kila siku. Khofu hii ilimalizika pale tu sheriya ilipokamilika, pale Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipoaga dunia.

2. **IDADI YA SAWA KATIKA SUNNAH NI KUMI NA MOJA:** Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliswali rakaa'ah kumi na moja katika swala ya Taraweeh. Hadeeth yenye madai yakwamba aliswali rakaa'ah ishirini ni dhaifu sana. Hairuhusiwi kuswali zaidi ya rakaa'ah kumi na moja, kwa sababu jambo hilo linakwenda kinyume na kitendo chake na amri yake, **<Swalini kama mulivyoniona mimi nikiswali>**. Kwa ajili hii, hairuhusiwi kuongeza kwenye sunnah ya Fajr au nyenginezo.

3. **RAI YETU JUU YA WALE WENYE KUKATAA:** Kwa wale wenye kuswali zaidi ya rakaa'ah kumi na moja katika swala ya Taraweeh, sisi hatuwazingatii wao kuwa ni wazushi wala wapotofu - iwapo msimamo wao umetokana na kufahamikiwa na Sunnah hiyo ki-makosa, au haikuwadhihirikia, na wala sio kwamba ati wamefuata hawaa za nafsi zao.

4. SUNNAH NI BORA KULIKO HIYO NYONGEZA: Hata kama mtu atakubali yakwamba inaruhusiwa kuongeza idadi ya taraweeh, hapana shaka yakwamba ni bora kushikamana na idadi ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyoiswali, kwa sababu alisema, **<Uongofu ulio bora ni ule wa Muhammad>.**

5. **'UMAR ALIIHUISHA SUNNAH:** 'Umar (رضي الله عنه) hakuzua katika swala ya taraweeh; bali aliihuisha sunnah ya kuiswali kwa jamaa'ah; na akaidumisha idadi ya rakaa'ah zake kulingana na sunnah. Chochote kilichopokewa tafauti kutoka kwake si swaheeh katika mapokezi yake yote (au silsila zake za upokezi); na silsila hizo ni kiasi cha kwamba hazisaidiani zenyewe kwa zenyewe.

6. **MASWAHABA HAWAKUSWALI RAKAA'AH ISHIRINI:** Haikuthubutu yakwamba yoyote miongoni mwa Maswahaba aliwahi kuswali rakaa'ah ishirini katika swala ya taraweeh. Kwahivyo, inampasa mtu kushikamana na idadi ya rakaa'ah zilizothubutu katika sunnah na kuthibitishwa na 'Umar (رضي الله عنه). Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametuamrisha sisi tufuate sunnah zake na sunnah za Makhulafaa waongofu.

7. **HAPANA RUHUSA YA KUONGEZA:** Hata kama tutachukulia yakwamba kuongeza juu ya idadi iliyo swaheeh imeswihi kupokewa kutoka kwa baadhi ya Maswahaba (jambo ambalo si kweli), itatubidi kuzingatia yakwamba ilikuwa ni kwa sababu fulani isiyokuwepo leo hii.

8. **WANAVYUONI WAMEKANUSHA NYONGEZA:** Kuswali zaidi ya rakaa'ah kumi na moja kumekanushwa na Maalik, Ibn al-'Arabi na wanavyuoni wengine. Zaidi ya hayo, hakuna *'ijmaa'* (maafikiano) kabisa kuhusu rakaa'ah ishirini miongoni mwa Maswahaba au wanavyuoni wakubwa.

9. **MSIMAMO WA WANAVYUONI WAKUBWA:** Kukataa rakaa'ah za ziyada hakumaanishi kuwakanusha wanavyuoni waheshimiwa wenye kukubali ziyada hiyo. Kukhitilafiana nao kwenye mas'ala haya hakumaanishi, kwa njia yoyote, kudunisha 'ilmu yao na ufahamu wao.

10. **KUPOTEZA KHUSHOO':** Kusisitiza ziyada kwenye idadi iliyopokewa kumewazidisha watu kuswali kwa haraka, wakapoteza khushoo', na kwa mara nyingi, uswaheeh wa swala yenyewe.

11. **KUSWALI KWA IDADI YA CHINI YA KUMI NA MOJA:** Hata kama hairuhusiwi kuswali zaidi ya rakaa'ah kumi na moja, lakini inaruhusiwa kuswali idadi ya chini ya hapo, chini mpaka kiasi cha rakaa'ah moja. Hili limethubutu kwenye Sunnah na vitendo vya ma-Salaf.

12. **NJIA TAFAUTI ZA KUSWALI QIYAAM:** Njia zote tafauti ambazo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alizoswali *qiyaam* na *witr* zinaruhusiwa. Njia bora ni kuswali rakaa'ah kumi na moja kwa kisimamo kirefu, na kutoa salaam baada ya kila jozi ya rakaa'ah.

13. **HATIMAE:** Yafuatayo ni maneno ambayo kwayo, Sheikh al-Albâni (رحمه الله) aliyoyamalizia kuhusu *Swalaat ut-Taraweeh*:

Huu ndio mwisho wa yale ambayo Allâh Aliyonirahisishia mimi katika ukusanyaji wa mada hii ya swala ya taraweeh. Lau kama nilikuwa sawa, basi hayo yametokana na Allâh (سبحانه وتعالى), ambaye Utukufu na Ne'ma zote ni zake. Na lau kama uwezekano mwengine, basi mimi namsihi kila mmoja atakaeona makosa anitanabahishe; na Allâh Atamlipa mema. Utukufu ni wako, Yaa Allâh , kila sifa njema zinakuthubutukia Wewe; Nashuhudia yakwamba hapana mola anaestahiki kuabudiwa kwa hakki isipokuwa Wewe; Naomba msamaha kutoka kwako; Namuomba Allâh amfikilizie swala na salaam Mtume asiyekuwa akijua kusoma wala kuandika, na kwa jamii yake yote na Maswahaba zake. Na mwisho wa ulinganizi wetu ni, *al-Hamdu lillaah Rabbil 'aalameen."*

I'TIKÂF

Na: Sheikh al-Halabi na al-Hilaalee

Hikma Yake: Ibn al-Qayyim amesema: "Kwa vile kutengenekewa kwa moyo na kuwa imara kwake juu ya njia ya kuelekea kwa Allâh (سبحانه وتعالى) hutegemea juu ya muelekeo wake kwa Allâh Peke yake na kuusababisha kugeuka na kumtafakari Allâh (سبحانه وتعالى) Kwa vile maradhi ya moyo hayawezi kuponywa isipokuwa kwa kumuelekea Allâh (سبحانه وتعالى) na maradhi yake yatazidi kwa kunywa na kula sana, kuchanganyikana na watu kupita kiyasi, kusema sana na kulala sana. Mambo haya huusababisha (moyo) kuzurura kwenye kila bonde, na kuukatiza kutoka kwenye njia yake ya kuelekea kwa Allâh, na kuudhoofisha, ukaupoteza njia au akukomesha.

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

Kutokana na Rehma za Mtenza Nguvu na Mwenye Huruma kwa waja wake ni kwamba aliwafaradhishia wao saumu, ambayo itakayokomesha ziyada za kula na kunywa, na kuusafisha moyo na matamaniwa yake yenye kuupoteza kwenye safari yake ya kuelekea kwa Allâh (سبحانه وتعالى). Aliwafaradhishia kwa kadiri ya maslahi yenye kumnufaisha mja, katika dunia yake na akhera yake, na haitomdhuru, wala kuharibu yaliyo na maslahi nae. Vilevile aliwafaradhishia *I'tikâf*, yenye malengo yaliyokusudiwa kuufanya moyo uwe ni wenye kushughulika kikamilifu na Allâh, na kujikusanya kwa Allâh Pekee, na kuuweka faragha na Allâh (سبحانه وتعالى) na kujikatiza kutokana na kushughulika na viumbe. Na kujishughulisha na Allâh Peke Yake, ambaye Aliye-epukana na kila upungufu, kiyasi cha kwamba kumkumbuka Yeye, kumpenda Yeye na kumuelekea Yeye ikachukuwa mahali pa hamu zote za moyo na mapendekezo yake, mpaka akawa na uwezo wa kuyashinda. Kwahiyo mambo yake yote ni kwa ajili Yake. Fikra Zake zote ni zenye kumkumbuka Yeye, na kufikiria njia za kujipatia radhi Zake na mambo yatakayosababisha mkuruba Naye. Hayo humpelekea akapumbazika na Allâh badala ya watu, kwahivyo hayo humtayarisha yeye akawa kwenye amani na Yeye Peke yake katika siku ya upweke kwenye kaburi, wakati ambao hapatokuwa na yoyote atakaekupumbaza, wala hapatokuwa na yoyote atakaekumliwaza wala kumfurahisha isipokuwa Yeye. Kwahivyo hili ndilo lengo kubwa la *I'tikâf*."

Maana Yake: Maana yake ni kujifungamanisha nafsi yako kikamilifu na kitu, kwahiyo linatumika kumueleza mwenye kujizoezesha na msikiti na kufanya ibada ndani yake.

Uwajibu Wake: Imependekezwa katika mwezi wa Ramadhân na katika masiku mengine ya mwaka, kwani imethubutu yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alifanya *I'tikâf* katika siku kumi za mwisho wa (mwezi wa) Shawaal.

Pia 'Umar alimwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Ewe Mjumbe wa Allâh, mimi nilikuwa nimeweka nadhiri katika wakati wa Jaahiliyyah yakwamba nitakaa *I'tikâf* kwa usiku mmoja katika msikiti Mtukufu (al-Masjidul-Haraam)?" Akamjibu: "Basi tekeleza nadhiri yako [na ufanye *I'tikâf* kwa usiku mmoja]."

Hatahivyo, ni bora zaidi katika mwezi wa Ramadhân kutokana na hadeeth ya Abu Hurairah (رضي الله عنه) "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifanya *I'tikâf* kwa siku kumi kila ifikapo Ramadhân, kisha ulipokuwa ni mwaka ambao alipochukuliwa, alifanya *I'tikâf* kwa siku ishirini."

Wakati bora ni mwisho wa Ramadhân, kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) "Alikuwa akifanya *I'tikâf* katika siku kumi za mwisho za Ramadhân mpaka Allâh **(** عزّ وجلّ**)** alipomchukuwa."

Shuruti Zake: Haikuwajibishwa isipokuwa kwenye misikiti, kama alivyosema Allâh (سبحانه وتعالى)

"Wala msiwaingilie wanawake zenu haliyakuwa nyinyi muko kwenye *I'tikâf* msikitini…"

Misikiti iliyotajwa hapa na isichukuliwe kutokuwa na mipaka kwani shuruti zake zimetokea kwenye Sunnah iliyo swaheeh, na ni maneno yake (صلى الله عليه وسلم) "Hakuna *I'tikâf* isipokuwa kwenye misikiti mitatu."

Sunnah kwa mwenye kufanya *I'tikâf* ni kwamba na afunge saumu kama ilivyopokewa kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنها)

Mambo Yanayoruhusiwa Kwa Mwenye Kukaa *I'tikâf*

Inaruhusiwa kwa aliye kwenye *I'tikâf* kutoka msikitini kwa haja fulani, na anaruhusiwa kujiegemeza nje ya msikiti kwa ajili ya kutoa kichwa chake nje ya msikiti kwa ajili ya kuoshwa na kuchanwa nywele zake. Amesema 'Aaisha (رضي الله عنها): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akinitolea kichwa chake alipokuwa (akikaa *I'tikâf*) msikitini (nami nilikuwa chumbani mwangu) nami nilikuwa nikizichana (na kwenye riwaya nyengine: nikiziosha nywele zake) [na kizingiti cha mlango kilikuwa baina yetu] [nami nilikuwa kwenye heidh] nae alikuwa haingii nyumbani isipokuwa kwa mahitaji [ya mtu], alipokuwa akikaa *I'tikâf*."

Inaruhusiwa kwa mwenye kukaa *I'tikâf* na kwa wengine watawadhe msikitini kutokana na maneno ya mtu aliyekuwa akimuhudumikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitawadha wudhoo' ambao ni khafifu."

Aweza mtu kujenga kijihema kidogo ndani ya msikiti katika sehemu ya nyuma, na akakaa *I'tikâf* ndani yake, kwani 'Aaisha (رضي الله عنها) alikuwa akimuekea Mtume (صلى الله عليه وسلم) kijihema kidogo alipokuwa akikaa *I'tikâf* na hili lilikuwa kama alivyoamrisha.

Aweza kuweka matandiko yake na godoro lake hapo ndani kutokana na aliyoyasema Ibn 'Umar (رضي الله عنها) kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) "Yakwamba alipokaa *I'tikâf*, alikuwa akiwekewa matandiko au godoro lake nyuma ya nguzo ya toba."

I'tikâf Ya Mwanamke, Na Kumzuru Mumewe Msikitini

Yafaa kwa mwanamke kumzuru mumewe ambaye anaefanya *I'tikâf*, na anaweza kutembea nae mpaka kwenye mlango wa msikiti. Amesema Swafiyyah (رضي الله عنها) Mtume (صلى الله عليه وسلم) alifanya *I'tikâf* [katika kumi la mwisho wa Ramadhân], basi nikamuendea kumzuru katika wakati wa usiku [na alikuwa na wakeze kisha wakaondoka]. Nikazungumza nae kwa muda, kisha nikasimama kutaka kuondoka, [basi akasema: "Usifanye haraka kwa sababu mimi nitakushindikiza." Akasimama pamoja na mimi ili anishindikize – na makaazi yake (bibi Swafiyyah) yalikuwa ni kwenye nyumba ya Usaamah Ibn Zayd [mpaka alipoufikia mlango wa msikiti karibu na mlango wa Umm Salamah], palikuwa na watu wawili wa kabila la Answaar wakipita, walipomuona Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakaanza kukaza mwendo, basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaambia: "Taratibuni kwani huyu ni Swafiyyah Bint Huyayy." Wakasema: "*SubhaanAllâh*! (Kutakasika ni kwa Allâh) Ewe Mjumbe wa Allâh!" Akasema: "Kwa hakika Shaitaan huzunguka ndani ya mwili wa mwana -adamu katika mishipa kama inavyozunguka damu, na mimi nilichelea yakwamba hwenda akawatia dhana mbaya." – au alisema "kitu – ndani ya nyoyo zenu."

Inaruhusiwa kwa mwanamke kukaa *I'tikâf* pamoja na mumewe au peke yake kama alivyosema 'Aaisha (رضي الله عنها): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akikaa *I'tikâf* katika kumi la mwisho wa Ramadhân mpaka Allâh alipomchukuwa, kisha wake zake walikaa *I'tikâf* baada yake."

Sheikh wetu [al-Albaani (رحمه الله) amesema: "Katika hadeeth hii kuna dalili ya kuruhusiwa kukaa *I'tikâf* kwa wanawake, na hapana shaka yakwamba jambo hilo limefungwa juu ya ruhusa za mawalii wao, na kwamba kunapatikana usalama kutoka kwenye fitna, na kutopatikana faragha wanaume – kwa sababu ya dalili nyingi (zenye kukataza) hayo, na msingi wa hukmu za ki-fiqh hapa ni kwamba kuzuiya ufisadi hutangulizwa kuliko kuleta maslahi."